Hekima, Umoja, Amani, Ni ngao Zetu!

# NCHI YETU

Tanzania Imara, Kazi na Utu

www.maelezo.go.tz Toleo Na. 975 | 03 Machi, 2026 | Idara ya Habari MAELEZO




HALIUZWI



# Ujenzi Matenki ya Mafuta Bandari ya Dar es Salaam

## Kufungua Fursa za Kiuchumi

**Na Bupe Mwaiseje – MAELEZO**

Tanzania imeandika ukurasa mpya katika sekta ya bandari baada ya kuzindua mradi mkubwa wa ujenzi wa matenki ya kisasa ya kupokea na kuhifadhi mafuta katika Bandari ya Dar es Salaam, mradi unaotajwa kuwa kichocheo kipya cha ukuaji wa uchumi wa taifa.

Akizindua ujenzi wa mradi huo leo Machi 3, 2026 Jijini Dar es salaam katika hafla iliyohudhuriwa na viongozi mbalimbali wa Serikali na sekta binafsi, Rais wa wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Dkt. Tanzania, Samia Suluhu Hassan, amesema hatua hiyo ni sehemu ya mkakati wa kuifanya Tanzania kuwa kitovu cha biashara na uwekezaji katika ukanda wa Afrika Mashariki na Kati.

“Ndugu viongozi na wananchi, bandari yetu ya Dar es Salaam ina mchango mkubwa sana katika kukuza uchumi wa nchi yetu na ustawi wa wananchi,” amesema Rais Samia huku akisisitiza kuwa maboresho yanayoendelea tayari yamezaa matunda.

Rais Samia amesema, mapato ya Serikali kupitia kodi ya forodha yameongezeka kwa kasi, kutoka Shilingi trilioni 7.3 mwaka 2020/2021 hadi kufikia Shilingi trilioni 12.31 mwaka 2024/2025 ishara ya mafanikio ya mageuzi yanayoendelea bandarini.

Aidha, Rais Samia ametoa maelekezo kwa Wizara ya Uchukuzi kuhakikisha mradi huo unatekelezwa kwa haraka na Mamlaka ya Usimamizi wa Bandari Tanzania (TPA) kuimaisha mfumo wa uhakiki wa ufuatiliaji ili kuongeza uwazi na uwajibikaji.

Mkurugenzi Mkuu wa Mamlaka ya Usimamizi wa Bandari Tanzania (TPA) , Plasduce Mkeli Mbossa, amesema mradi huo wenye thamani ya Shilingi Bilioni 678.641 unatarajiwa kuongeza fursa za ajira kwa Watanzania, kupunguza siku za kushusha mizigo, kuongeza mapato, kuondoa gharama za kusubiria mafuta kwa muda mrefu bandarini na kuongeza fursa za wafanyabishara.

“Mradi huu utaleta mageuzi makubwa katika Bandari ya Dar es Salaam, Kupunguza muda wa kuhudumia mizigo, kuongezeka kwa mapato ya Serikali na ajira kwa wananchi. Hii ni dalili kwamba Tanzania inaimarisha nafasi yake kama lango kuu la biashara katika ukanda huu” amesema.



# Rais Samia Aagiza Kuimarishwa kwa Akiba ya Mafuta Kukabili Misukosuko ya Bei Duniani

**Na. Naishooki Makeseni - MAELEZO**

Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan, ameiagiza Wizara ya Uchukuzi kuimarisha akiba ya kimkakati ya mafuta ili kuongeza uthabiti wa taifa dhidi ya misukosuko ya kimataifa inayoathiri bei ya nishati katika soko la dunia.

Akizungumza leo Machi 3, 2026 jijini Dar es Salaam wakati wa uwekaji wa jiwe la msingi wa mradi wa ujenzi wa matanki ya kupokea na kuhifadhi mafuta katika eneo la Kigamboni, Rais Samia amesema Tanzania haina budi kujiandaa mapema kukabili changamoto za mabadiliko ya bei yanayosababishwa na migogoro ya kimataifa.

Ameeleza kuwa misukosuko iliyojitokeza wiki iliyopita katika baadhi ya nchi tayari imechangia kupanda kwa bei ya mafuta kwa takribani asilimia 13, hali inayoweza kuathiri gharama za maisha na uendeshaji wa shughuli za kiuchumi.

“Tumuombe Mungu watu wale wakae mezani wazungumze, wakubaliane, misukosuko hii iishe ili dunia irudi katika hali yake ya kawaida ya kuendesha chumi za nchi zetu,” amesema Rais Samia.

Rais Samia amesisitiza kuwa uwekezaji katika miundombinu ya kisasa ya kuhifadhi mafuta ni hatua ya kimkakati ya kuimarisha usalama wa nishati nchini na kulinda uchumi dhidi ya athari za mabadiliko ya ghafla ya bei katika soko la kimataifa.

Aidha, ameongeza kuwa hatua hiyo ni sehemu ya mkakati mpana wa Serikali wa kuhakikisha upatikanaji wa nishati unakuwa wa uhakika, nafuu na endelevu kwa maendeleo ya viwanda, biashara na ustawi wa wananchi.

Mradi huo wenye uwezo wa kuhifadhi mita za ujazo 374,000 ambazo ni sawa na Lita milioni 378, unatarajiwa kuongeza uwezo wa taifa kuhifadhi akiba ya kimkakati, kupunguza utegemezi wa ununuzi wa dharura na kusaidia kudhibiti mishtuko ya bei kwa walaji wa ndani.



# Rais Samia: Tanzania Kutumia Jiografia Yake Kuwa Lango Kuu la Biashara Afrika

**Na. Naishooki Makeseni - MAELEZO**

Rais wa wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan, amesema Serikali imejipanga kikamilifu kutumia nafasi ya kijiografia ya nchi kama lango kuu la biashara kwa ajili ya kuhudumia mataifa yasiyo na bandari pamoja na yale yaliyounganishwa na Bahari ya Hindi katika ukanda wa Afrika na kimataifa.

Rais Samia amesema hayo wakati akiweka jiwe la msingi la ujenzi wa matanki ya kupokea na kuhifadhi mafuta katika eneo la Kigamboni, jijini Dar es Salaam, akisisitiza kuwa mkakati huo ni sehemu ya Dira yaTaifa kuifanya Tanzania kuwa kitovu cha biashara na usafirishaji barani Afrika.

“Maboresho yote yaliyofanyika katika sekta ya uchukuzi kwa bandari zetu yameongeza uwezo wa bandari kuhudumia meli kubwa, zikiwemo za aina ya Post-Panamax, na kuongeza ushindani dhidi ya bandari nyingine duniani,” amesema Rais Samia.

Ameeleza kuwa hapo awali Tanzania haikuwa na uwezo wa kupokea meli kubwa zinazotia nanga katika bandari kuu za kimataifa, lakini hali imebadilika kufuatia uwekezaji mkubwa katika miundombinu ya bandari, hususan katika Bandari ya Dar es Salaam.

Rais Samia ameongeza kuwa dhamira ya Serikali ni kuhakikisha Tanzania inakuwa na mazingira salama, ya kisasa na yenye ushindani wa kimataifa kwa ajili ya kupokea meli za ukubwa wowote akibainisha kuwa juhudi hizo zitaimarishwa zaidi baada ya kukamilika kwa ujenzi wa Bandari ya Bagamoyo, ambao unatarajiwa kuongeza uwezo wa nchi kuhudumia mizigo kwa kiwango kikubwa zaidi.

Kwa kutumia vyema nafasi ya kijiografia ya Tanzania, Rais amesema nchi itaongeza mapato ya Serikali, kuvutia uwekezaji mpya na kuimarisha ushirikiano wa kibiashara na mataifa jirani yasiyo na bandari huku ikichochea ukuaji wa uchumi wa taifa na kuimarisha ustawi wa ukanda mzima.



# Mradi wa Matanki ya Mafuta Kuifanya Tanzania Kitovu cha Biashara Kikanda

**Na. Rajabu Sodangu – MAELEZO**

Rais wa Tanzania wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Samia Suluhu Hassan, amesema mradi wa ujenzi wa matanki ya mafuta katika Bandari ya Dar es Salaam utakuwa chachu ya kuimarisha uchumi wa taifa na kuifanya Tanzania kuwa kitovu cha biashara na maendeleo kwa nchi jirani.

Rais Samia ametoa kauli hiyo katika hafla ya uwekaji wa jiwe la msingi la mradi wa ujenzi wa matanki 15 ya kupokea na kusambaza mafuta, iliyofanyika leo Machi 3, 2026 katika viwanja vya Madani, Wilaya ya Kigamboni jijini Dar es Salaam.

Amesema Serikali kupitia Mamlaka ya Usimamizi wa Bandari Tanzania (TPA) imeanza ujenzi wa matanki hayo yenye ujazo wa mita za ujazo 374,000, kwa gharama ya Shilingi bilioni 664.6 na unatarajiwa kukamilika ndani ya miezi 24, ifikapo Februari 2027 ambapo hadi sasa umefikia asilimia 41 ya utekelezaji.

Rais Samia amesema uwekezaji huo wa Serikali ni hatua ya kimkakati katika kuimarisha nafasi ya Tanzania kama lango la biashara na uwekezaji wa kikanda na kimataifa. "Uwekezaji wa Serikali katika ujenzi wa matanki ya kupokea mafuta ni hatua ya kimkakati katika kuimarisha nafasi ya Tanzania kama kitovu cha biashara na uwekezaji wa kibiashara wa kikanda na kimataifa," amesema Rais Samia.

Ameongeza kuwa kukamilika kwa mradi huo kutapunguza muda wa meli kusubiri kuhudumiwa bandarini, kupunguza msongamano, kuongeza ufanisi katika utoaji huduma na hatimaye kuongeza mapato ya taifa kupitia ushuru wa forodha.

Sambamba na hilo, Rais Samia ameiagiza Wizara ya Uchukuzi kupitia Mamlaka ya Usimamizi w Bandari Tanzania (TPA) kuhakikisha mradi unakamilika kwa wakati, kwa ubora unaozingatia viwango vya kimataifa na kwa kuzingatia utunzaji wa mazingira, akisisitiza kuwa mradi huo utaimarisha usalama wa uhifadhi wa mafuta nchini.

Aidha, ameitaka Wizara ya Nishati kujiimarisha kimkakati katika uhifadhi wa mafuta ili kuongeza uwezo wa nchi kukabiliana na misukosuko ya kimataifa, ikiwemo kupanda kwa bei ya mafuta duniani.




# Dr.Kijaji : Tanzania Yaendelea Kung'ara Kimataifa Na Kuwa Kituo Bora Cha Utalii na Uhifadhi Duniani

**Na. Calvin Katera - Arusha.**

Waziri wa Maliasili na utalii nchini Dkt. Ashatu Kijaji (Mb) amesema kuwa Tanzania imeendelea kuwa kituo bora cha utalii Duniani kutokana na wingi wa Tuzo inazoendelea kuzipokea kupitia taasisi na majukwaa ya kimataifa. Hali hii imechagizwa na ulinzi imara unaofanya na maafisa na askari wa Jeshi la Uhifadhi na Misitu nchini.

Kauli hiyo aliitoa leo machi 03, 2026 katika Kilele cha Maadhimisho ya Siku ya Wanyamapori Duniani iliyofanyika Kitaifa katika Viwanja vya Nanenane vilivyopo Njiro jijini Arusha.

Katika hafla hiyo Dkt. Kijaji alisema, "Tanzania imeendelea kung'ara kimataifa kwa kuwa kituo bora cha utalii duniani. Hali hii inathibitishwa na uwepo wa tuzo tunazoendelea kuzipata kupitia taasisi na majukwaa mbalimbali duniani. Hivi karibuni tumeshinda tuzo tano muhimu za utalii duniani, hakika sote tunapaswa kuendelea kutambua mchango mkubwa wa Rais wetu Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kunadi vivutio hivyo."

Sambamba na hilo Dkt. Kijaji aliongeza kuwa mafanikio hayo yanatokana na usimamizi madhubuti wa maeneo ya hifadhi, mapambano dhidi ya ujangili pamoja na ushirikishwaji wa jamii katika kulinda na kuhifadhi maliasili.

"Wizara kupitia taasisi zake za TANAPA, TAWA, TFS na NCAA zitaendelea kuimarisha mifumo ya ulinzi na matumizi sahihi ya teknolojia ili kuhakikisha maliasili hizo zinaendelea kuwa na mchango katika uchumi wa Taifa letu", aliongeza Dkt. Kijaji.

Kwa upande wake, Mkurugenzi wa Wanyamapori nchini, Dkt. Alexander Lobora alisema kuwa kuimarika kwa hali ya wanyamapori nchini ni matokeo ya ushirikiano kati ya serikali, wadau wa uhifadhi na wananchi wanaozunguka maeneo ya hifadhi.

Aidha, Dkt. Lobora alisema, "Ikolojia ya mimea imeimarika, halikadhalika idadi ya wanyamapori imeongezeka kutokana na matumizi ya TEHAMA, jambo linaloendelea kuipa Tanzania heshima katika medani za kimataifa."

Naye, Naibu Katibu Mkuu wa Wizara ya Maliasili na Utalii Bw. Nkoba Mabula, alisema kuwa wizara itaendelea kusimamia sera na mikakati itakayohakikisha uhifadhi unaenda sambamba na maendeleo ya wananchi.

Hata hivyo Bw. Mabula, aliendelea kusisitiza kuwa uchumi wa jamii na uhai wa mfumo wa ikolojia haviwezi kutenganishwa na siku hii. Maadhimisho ya Siku ya Wanyamapori Duniani ni jukwaa la kuwasemea wanyamapori hao wasioweza kujisemea wenyewe.

Maadhimisho hayo yaliyobeba kauli mbiu isemayo "Mimea Dawa na Manukato: Kutunza Afya, Kuhifadhi Urithi na Kuboresha na Maisha" pia ilihudhuliwa na Mhe. Joseph Mkude Mkuu wa Wilaya ya Arusha, Mwenyekiti wa CCM Mkoa wa Arusha, Wakurugenzi kutoka Wizara ya Maliasili na Utalii, Makamishna wa Uhifadhi kutoka TANAPA, NCAA, TAWA, Makamishna Waandamizi, Maafisa na Askari wa Jeshi la Uhifadhi na Misitu, Wakuu wa Vyuo na Taasisi, Viongozi wa Dini na wadau mbalimbali kutoka sekta ya Uhifadhi na Utalii.



# Serikali Yapunguza Masharti ya Mikopo kwa Vijana.

**Na Mwandishi Wetu**

Serikali imetangaza kupunguza masharti ya upatikanaji wa mikopo ya Mfuko wa Maendeleo ya Vijana, ikiwemo kuondoa sharti la lazima la kuunda kikundi ili kijana aweze kukopa.

Akizungumza wakati wa ufunguzi wa Kongamano la Vijana mkoani Mtwara, Waziri wa Ofisi ya Rais – Maendeleo ya Vijana, Dkt. Joel Nanauka, amesema hatua hiyo inalenga kuhakikisha kila kijana ananufaika na mikopo hiyo bila vikwazo.

Kongamano hilo, limeambatana na vijana kukabidhiwa bajaji, pikipiki na maguta yenye thamani ya Shilingi milioni 140 kupitia Benki ya CRDB Foundation kama sehemu ya mkakati wa kuwawezesha kiuchumi.

Dkt. Nanauka amesema Serikali imetoa muda wa miezi 3 hadi 6 kabla ya mkopaji kuanza kurejesha mkopo ili kurahisisha mtiririko wa marejesho na kuepusha vijana kukimbilia mikopo yenye riba kandamizi(kausha damu)

Mkuu wa Mkoa wa Mtwara, Kanali Donald Msengi, amewataka vijana kutumia vyema fursa hiyo ili kuwa mfano kwa wengine, huku Meneja wa Biashara wa CRDB Kanda ya Kusini, Emmanuel Biganio, akisisitiza kuwa benki hiyo imejipanga kuongeza kasi ya utatuzi wa changamoto za wananchi.




# Mkazi wa Manyara Aliyemuomba Waziri Mkuu Kupandikizwa Figo Aanza Matibabu BMH

**Na Ludovick Kazoka - BMH - Dodoma**

Mkazi wa Mkoa wa Manyara, Bi Juliana Francis, ameanza rasmi matibabu ya kupandikizwa figo katika Hospitali ya Benjamin Mkapa (BMH), kufuatia maelekezo ya Waziri Mkuu wa Tanzania, Mwigulu Mchemba.

Bi Juliana alimwomba Waziri Mkuu apatiwe huduma ya upandikizaji figo katika hospitali hiyo ya rufaa ya kanda ya kati, ombi ambalo lilipokelewa na kutekelezwa mara moja kwa kuagiza aanze kupatiwa matibabu.

Akizungumza kuhusu hatua hiyo, Mkurugenzi wa Tiba wa BMH, Dkt. Jesse Jonathan, amesema hospitali hiyo imepokea maelekezo ya Waziri Mkuu na tayari mgonjwa ameanza mchakato wa matibabu. "Tumepokea maelekezo ya Mheshimiwa na tayari ameanza matibabu," amesema Dkt. Jonathan.

Kwa sasa Bi Juliana anaendelea na huduma ya kusafisha damu (dialysis) ikiwa ni sehemu ya maandalizi ya upandikizaji figo unaotarajiwa kufanyika katika hospitali hiyo.

Akizungumza akiwa wodini wakati wa matibabu, Bi Juliana alitoa shukrani kwa uongozi wa BMH na Serikali kwa kumwezesha kupata huduma hiyo muhimu. "Nawashukuru BMH kwa matibabu," amesema.

Hatua hiyo inaonesha juhudi za Serikali katika kuimarisha huduma za kibingwa nchini, hususan katika hospitali za rufaa, ili wananchi waweze kupata matibabu ya kibingwa ndani ya nchi bila kulazimika kusafiri nje ya mipaka ya Tanzania.



# Mhe.Silinde: Serikali Kuendeleza Kilimo Ikolojia Hai kwa Usalama wa Chakula na Mazingira

**Na. Mwandishi Wetu**

Naibu Waziri wa Kilimo, Mhe. David Silinde, amesema Serikali itaendelea kushirikiana na wakulima wanaojishughulisha na kilimo ikolojia hai ili kufikia malengo ya kilimo endelevu, kuongeza uzalishaji na kuhakikisha utoshelevu wa chakula kwa kuzingatia utunzaji wa mazingira.

Silinde alitoa kauli hiyo jijini Dodoma Machi 3,2026 wakati akimwakilisha Waziri wa Kilimo, Mhe. Daniel Chongolo, katika Mkutano wa Nne wa Kitaifa wa Kilimo Ikolojia Hai (National Ecological Organic Agriculture Strategy - NEOAS).

Ametoa wito kwa wadau wa sekta ya kilimo kuendelea kufadhili utekelezaji wa mkakati huo chini ya uratibu wa Kikosi Kazi cha Utekelezaji (National Implementation Task Force - ITF) ili kuleta mageuzi makubwa katika sekta hiyo akiongeza kuwa lengo ni kupunguza umaskini, kuongeza ajira hasa kwa vijana na wanawake, na kufikia ukuaji wa sekta ya kilimo kwa asilimia 10 ifikapo mwaka 2030.

Akizungumzia kaulimbiu ya mkutano huo, “Kilimo Ikolojia Hai: Kuimarisha Usalama wa Chakula na Lishe, Uhimilivu na Ustahimilivu wa Kiuchumi,” Mhe. Silinde amesema inaendana na vipaumbele vya Wizara ya Kilimo pamoja na mipango ya maendeleo ya sekta hiyo. Amebainisha kuwa Serikali imeongeza bajeti ya kilimo hadi kufikia Shilingi trilioni 1.24 kwa mwaka wa fedha 2025/2026, ikiwa ni sehemu ya mapinduzi ya kilimo nchini.

Aidha, amewataka washiriki wa mkutano kujadili kwa kina utekelezaji wa Mkakati wa Kilimo Ikolojia Hai wa mwaka 2023–2030 pamoja na Mpango Kabambe wa Mageuzi ya Kilimo 2050 (Agriculture Master Plan 2050), ili kuhakikisha Tanzania inafikia malengo ya kilimo endelevu na usalama wa chakula kwa kuzingatia hifadhi ya mazingira.

Katika hatua nyingine, Mhe.Silinde amesema Tanzania ina jumla ya mbegu za asili 770 za mazao mbalimbali ikiwemo ulezi, mpunga, mtama, uwele, migomba, maharage na papai. Kupitia Taasisi ya Kudhibiti Ubora wa Mbegu Tanzania (TOSCI), aina 13 za mbegu za asili za mahindi, mpunga, maharage na papai zimetambuliwa na kuingizwa kwenye mfumo rasmi wa mbegu.

Vilevile, Taasisi ya Utafiti wa Kilimo Tanzania (TARI) inaendelea kukusanya, kusafisha na kutunza aina 360 za mbegu za asili za mazao mbalimbali ikiwemo mpunga, ufuta, uwele, ulezi, choroko, kunde, migomba, korosho, viazi vitamu, pilipili manga, tango, mbaazi na soya.

Hatua hizo zinaelezwa kuwa ni sehemu ya juhudi za Serikali za kulinda urithi wa mbegu za asili, kuimarisha kilimo hai na kuhakikisha wakulima wanazalisha kwa tija huku wakihifadhi mazingira kwa vizazi vijavyo.




# Wakulima Wanahimizwa Kutumia Mbolea kwa Wakati na Kwa Usahihi Kuongeza Mavuno na Kipato.

**Na Mwandishi Wetu**

Mkurugenzi Mkuu Kampuni ya Mbolea Tanzania, Samuel Mshote amesema kampuni hiyo inaendelea na zoezi la usambazaji na uuzaji wa mbolea kwa bei ya ruzuku kwa wakulima wote nchini, ikiwa ni sehemu ya jitihada za Serikali ya Tanzania kuongeza uzalishaji na tija katika sekta ya kilimo huku ikiwahimiza wakulima kutumia mbolea ya ruzuku kuzalisha kwa tija na kuongeza kipato

Amesema katika Kituo cha Mauzo cha Kibaigwa kilichopo mkoani Dodoma, jumla ya tani 109 za mbolea ya kupandia mazao aina ya Di-Ammonium Phosphate (DAP) zimepokelewa na tayari zimesambazwa kwa wakulima waliosajiliwa kwenye mfumo wa pembejeo za ruzuku.

Hatua hiyo inaendelea kuwawezesha wakulima kupata pembejeo bora kwa gharama nafuu, hivyo kuchochea uzalishaji wenye tija na kuimarisha usalama wa chakula nchini.



# TAWIRI Yaelekezwa Kuongeza Kasi Kudhibiti Migongano ya Binadamu na Wanyamapori

**Na Mwandishi Wetu**

Waziri wa Maliasili na utalii nchini Dkt. Ashatu Kijaji (Mb) ameitaka Taasisi ya Utafiti wa Wanyamapori Tanzania (TAWIRI) kukamilisha zoezi la kuwafunga tembo viongozi wa makundi mikanda ya visukuma mawimbi (GPS COLLARS) ili kufuatilia mienendo yao na kudhibiti Migongano kati yao na binadamu.

Dkt. Kijaji amesema hayo leo 03 Machi, 2026 katika Kilele cha Maadhimisho ya Siku ya Wanyamapori Duniani ambayo Kitaifa yamefanyika Viwanja vya Nanenane vilivyopo Njiro jijini Arusha.

Amesema kuimarika kwa Uhifadhi wa rasilimali za wanyamapori kumechochea ukuaji wa sekta ya utalii nchini. " idadi ya watalii imeongezeka kutoka 5,360,247 mwaka 2024 hadi watalii 5,935,561 mwaka 2025 sawa na ongezeko la asilimia 10.73" amefafanua Dkt. Kijaji

Dkt. Kijaji amesema Serikali inaendelea na mikakati ya kuhakikisha wanyamapori wanakuwa salama na watu wanakuwa salama "Wanyamapori ni rasilimali muhimu katika uchumi wa nchi ambapo kupitia utalii kumekuwa na ongezeko la fedha za kigeni kutoka Dola za Marekani Bilioni 3.9 hadi kufikia dola bilioni 4.4 sawa na ongezeko la asilimia 12.82."

Akibainisha changamoto za sekta ya uhifadhi, amesema Kuongezeka kwa migongano baina ya binadamu na wanyamapori wakali na waharibifu kunasababisha mahusiano hasi kati ya binadamu na wanyamapori " nielekeze kufanyika tafiti za kimkakati ili kubaini mbinu mpya za kukabiliana na changamoto hii" amehimiza Dkt.Kijaji

Aidha, amesema udhibiti wa migongano unaendelea ambapo tembo 176 viongozi wa makundi wamefungwa mikanda Ya visukuma mawimbi ili kufuatilia mienendo yao na kuthibiti uharibifu. Pia Kwa mamba na viboko tayari
vizimba 18 vimejengwa maeneo mbalimbali nchini

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**WIZARA YA MAMBO YA NJE NA USHIRIKIANO WA AFRIKA MSHARIKI**

**Dodoma**
02 Februari 2026

*Mawasiliano: gcu@nje.go.tz*

# TAARIFA KWA UMMA

## USHAURI WA HALI YA USALAMA NA USAFIRI KWA RAIA WA TANZANIA WANAOISHI AU KUSAFIRI MASHARIKI YA KATI

Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania inafuatilia kwa karibu hali ya usalama inayoendelea katika eneo la Mashariki ya Kati. Kutokana na mazingira ya kiusalama yanayoendelea, Serikali inatoa ushauri kwa raia wa Tanzania wanaoishi au wanaopanga kusafiri kwenda katika eneo hilo, ikiwemo Bahrain, Israel, Kuwait, Qatar, Falme za Kiarabu (UAE) na Oman.

Serikali inapenda kuwajulisha wananchi kuwa, kwa nyakati kama hizi, usaidizi wa kibalozi ana kwa ana unaweza kuwa na mipaka kulingana na eneo alipo mhusika na hali halisi ya kiusalama. Hivyo, raia wote wanahimizwa kuchukua tahadhari stahiki na kufuata maelekezo ya mamlaka husika.

Watanzania waliopo katika eneo la Mashariki ya Kati wanashauriwa kuzingatia maelekezo yafuatayo:

- Kuepuka kufanya safari za kwenda au kutoka Mashariki ya Kati katika kipindi hiki.
- Kubaki katika makazi mnayoishi inapowezekana.
- Kufuata maagizo yanayotolewa na mamlaka za maeneo husika na kuwa waangalifu wakati wote.
- Kuepuka maeneo yenye shughuli za usalama/kijeshi katika maeneo mnayoishi.
- Kutumia njia rasmi za mawasiliano na taarifa.
- Kuhifadhi pasipoti na vitambulisho vya Tanzania sehemu salama na inayopatikana haraka endapo kutatokea dharura.

Serikali inawasihi Watanzania walioko Mashariki ya Kati kujisitiri kwa uangalifu na kuendelea kufuatilia mawasiliano rasmi ya Ubalozi na ya dharura. Aidha, Watanzania wanaombwa kujisitiri kwa usajili kupitia kiunganishi kifuatacho kwa ajili ya ufuatiliaji wa karibu:
https://www.foreign.go.tz/forms/diaspora_middle_east_registration

Kwa dharura au maswali zaidi, wasiliana na Ubalozi wa Tanzania ulio karibu kama ifuatavyo:

Maelezo

# IDARA YA HABARI MAELEZO PODCAST